

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA NANE**

**12 APRILI, 2018**



## **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

### **MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**KIKAO CHA NANE – TAREHE 12 APRILI, 2018**

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**63. MHESHIMIWA RHODA EDWARD KUNCHELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Kuna mgogoro kati ya Manispaa na Wafanyabiashara wanaomiliki vibanda katika masoko ya Buzogwe Soko Kuu na Mpanda Hoteli ambapo Manispaa inawaongezea kodi Wafanyabiashara hao bila makubaliano ya pande zote mbili:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kumaliza mgogoro huo maana ni muda mrefu sasa na Wafanyabiashara wamefunga vibanda vyao

wakisubiri muafaka na hivyo Serikali kushindwa kukusanya kodi.

**64. MHESHIMIWA JOSEPHINE JOHNSON GENZABUKE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Zahanati nyingi za Vijiji vya Mkoa wa Kigoma katika Wilaya zote zina upungufu mkubwa sana wa Watumishi wa Afya na baadhi ya Zahanati hazina Waganga hivyo huduma zinatolewa na Manesi Wasaidizi tu:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Watumishi wa Afya wa kutosha katika maeneo hayo ili kuimarisha utoaji wa huduma za Afya Vijijini.

**65. MHESHIMIWA SAUL HENRY AMON (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Barabara ya Pakati-Njugilo-Masukulu- Matwebe hadi Mpakani ni barabara kubwa na inapita katika Kata nne ambazo ni Masoko, Bujela, Masukulu na Matwebe, Barabara hii ilishapandishwa daraja na kuwa ya TANROADS:-

Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa ili kuondoa adha kwa Wananchi kwa kupoteza kipato kwa mazao yao kuharibika njiani.

## **WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**

### **66. MHESHIMIWA JUMA KOMBO HAMAD (WINGWI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, Zanzibar ina nafasi gani katika Jumuiya za Kimataifa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **67. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:- Pamoja na kuishukuru Serikali kwa hatua mbalimbali zilizochukuliwa katika kumwondolea Mkulima matatizo ya zao la Tumbaku:-




- (a) Je, Serikali imechukua hatua zipi katika kuimarisha utendaji kazi wa Bodi mpya ya Tumbaku ili ifanye kazi kikamilifu;
- (b) Je, Serikali inawahakikishiaje Wakulima wa Tumbaku upatikanaji wa mbolea kwa wakati.

### III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI) NA  
WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA  
UTAWALA BORA):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

***(Majadiliano yanaendelea)***



**DODOMA  
12 APRILI, 2018**

**S. KAGAIGAI  
KATIBU WA BUNGE**